



**TANGAZO LA KAZI YA UJENZI**

Tarehe: 30.05.2019

1. Halmashauri ya Wilaya Nyasa, imepokea fedha kutoka Serikali Kuu, kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Bwalo, Jiko, Choo na Chumba cha Kubadilishia Nguo Katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kama ifuatavyo;
  - **UJENZI WA JENGO LA BWALO, JIKO, CHOO, SEHEMU YA KUNAWIA MIKONO NA CHUMBA CHA KUBADILISHIA NGUO SHULE YA SEKONDARI ENG. STELLA MANYANYA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA NYASA: KOTESHENI NA.LGA/145/2018-2019/W/EPVR/01**
2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Nyasa anawaalika mafundi wenye uzoefu wa Kujenga jengo tajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao.
3. Mchakato wa upatikanaji wa Mafundi utafanyika kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia Sheria za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2011 na mabadiliko yake ya Mwaka 2016.
4. Waombaji wenye nia ya kufanya kazi hii ya UJENZI, wanaweza kupata maelezo zaidi katika ofisi ya Manunuzi kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kwa siku za kazi tangia tarehe ya tangazo hili.
5. Nyaraka za maombi na michoro zinapatikana BURE Katika Ofisi ya Kitengo Cha Manunuzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa
6. Maombi yanatakiwa yaambatane na nakala mbili zilizojazwa vizuri na kufungwa kwenye bahasha na kuwasilishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P. 90, Mbamba-bay kabla ya tarehe 05-06-2018 Siku ya Jumanne saa 5:00 asubuhi.
7. Sifa za mwombaji, anatakiwa, ajue kusoma ramani na michoro ya nyumba, awe na vyeti vya mafunzo alivyosoma katika chuo chochote cha ufundi kinachotambulika, awe na uzoefu wa ujenzi wa majengo ya umma, awe na akaunti ya benki kwa ajili ya malipo ya kibenki, awe na idadi ya mafundi wasaidizi wasiopungua watano na vibarua wa kutosha.
8. Maombi yote yanatakiwa yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P. 90, Mbamba-Bay.
9. Fundi awe na uwezo wa kujenga, kumaliza nakukabidhi kazi kabla ya tarehe 15-10-2019. Pia mwombaji aambatanishe na mpango kazi.
10. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyo kamilika, maombi ambayo hayatakuwepo siku ya ufunguzi, hayatapokelewa na kuhusishwa na zoezi la uchambuzi wa kumpata fundi atakayefanya kazi ya ujenzi.

Jimson P. Mhagama  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA NYASA

